SEHEMU YA TANO
KANUNI ZA MAJADILIANO

Jinsi ya kupata nafasi ya kusema Bungeni

49.-(1) Mbunge akitaka kusema, aweza ama kumpelekea Spika ombi la maandishi, au kusimama kimya mahali pale, lakini hataanza kuzungumza mpaka Spika amwite ama kwa jina au kwa wadhifa wake, na kumruhusu kusema, na hapo ndipo ataanza kuzungumza, akielekeza maneno yake kwa Spika. Mbunge akimaliza kutoa maelezo yake atakaa kwenye nafasi yake, na hapo Spika atamwita Mbunge mwingine aliyempelekea ombi la maandishi, au kama Spika hakupata ombi lolote la maandishi, basi Mbunge mwingine yeyote anayetaka kulihutubia Bunge aweza kusimama mahali pake alipo. Iwapo Wabunge wawili au zaidi watasimama wakati mmoja, Spika atamwita yule Mbunge atakayemwona kwanza.

(2) Endapo maombi ya kuchangia katika hoja fulani yatakuwa mengi zaidi kuliko muda uliotengwa kwa kujadili hoja hiyo, Spika atazingatia kigezo kwamba Wabunge ambao bado hawajachangia katika hoja zilizotangulia kujadiliwa katika mkutano huo unaoendelea, au waliochangia mara chache zaidi wanapewa nafasi ya kwanza. Zaidi ya hapo, Spika atazingatia pia kwamba nafasi za kuchangia zitatolewa kwa uwiano unaofaa baina ya aina zote za Wabunge walioomba kuchangia hoja hiyo.

(3) Isipokuwa kama ameruhusiwa na Spika, Mbunge hatasoma hotuba yake; lakini kwa madhumuni ya kutilia nguvu maelezo yake anaweza kusoma madondoo kutoka katika kumbukumbu zilizoandikwa au kuchapishwa na anaweza pia kujikumbusha kwa kuangalia katika kumbukumbu alizoziandika.

(4) Kila Mbunge atasema akiwa amesimama, na atatoa maelezo yake hayo kwa kutumia vyombo vilivyowekwa kwa madhumuni ya kukuza sauti au kutafsiri. Kwa idhini ya Spika, Wabunge ambao kutokana na kilema au ugonjwa hawawezi kusimama, wanaweza kuzungumza wakati wamekaa.

(5) Iwapo wakati wa majadiliano Bungeni, Spika atasimama, Mbunge aliyekuwa anazungumza wakati huo ataketi na kukaa kimya ili Spika aweza kusikika bila matatizo.

(6) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni 104(1), hakuna Mbunge yeyote atakayeruhusiwa kuzungumzia suala lililokuwa likijadiliwa baada ya Spika kuwahoji, yaani baada ya uamuzi au idadi ya wanaoafiki na wasioafiki kujulikana.

(7) Mbunge hatazungumzia jambo lolote ambalo yeye mwenyewe ana maslahi ya kifedha nalo, isipokuwa baada ya kutaja jinsi anavyohusika, na kiwango cha maslahi hayo.

(8) Katika mjadala wowote, Mawaziri watatajwa kwa kutumia majina ya nyadhifa zao. Wabunge wengine wote watatajwa kwa kutumia neno "Mheshimiwa" kabla ya majina yao.

(9) Mbunge yeyote aweza pia kutoa maoni yake kwa maandishi, ambayo atampelekea Waziri au Mbunge mtoa hoja inayohusika, wakati ambapo hoja inaendelea kujadiliwa. Maoni hayo baadaye mtoa hoja anayehusika atayakabidhi kwa Katibu, ili yaweza kuingizwa katika Taarifa Rasmi.

(10) Kila Mbunge atalisemea lile jambo ambalo liko katika mjadala tu na hatarudiarudia maneno yake au yale yaliyokwisha kusemwa na Wabunge wengine. Kama ikitolewa hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja inayojadiliwa, mjadala sharti uwe juu ya hiyo hoja ya mabadiliko hayo mpaka imalizike, ndipo mjadala urudie kwenye ile hoja ya msingi.

Muda wa kusema Bungeni

49A. Muda wa kusema Bungeni umewekwa kwa lengo la kuwezesha Wabunge wengi zaidi wapate nafasi ya kuchangia mawazo yao. Kwa ajili hiyo isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo katika Kanuni hizi:-

(a) Kila Mbunge anayejadili hoja, ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika kumi na tano.
(b) Waziri anayetoa hoja, au anayehitimisha hoja yake, ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika sitini.
(c) Msemaji anayewasilisha maoni kwa mujibu wa Kanuni ya 43(5)(b) na (c), ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika thelathini.
(d) Mbunge anayetoa hoja binafsi ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika thelathini.

Mambo yasiyo-ruhusiwa Bungeni

50.-(1) Ni marufuku kabisa kusema uwongo Bungeni. Kwa sababu hiyo Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni, atawajibika kuwa na hakika kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi, na siyo mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu; na Spika au Mbunge mwingine yeyote, aweza kumdai Mbunge huyo atoe uthibitisho wa usemi wake. Mbunge aliyetakiwa kufanya hivyo atawajibika kutoa uthibitisho huo katika muda atakaopewa na Spika kwa ajili hiyo.

(2) Kila Mbunge atalisemea lile jambo ambalo, liko katika mjadala tu na hatarudia rudia maneno yake au yale yaliyokwisha kusemwa na Wabunge wengine. Iwapo Spika ametoa masuala zaidi ya moja, kwa mfano kama likitolewa suala la kufanya mabadiliko katika hoja inayojadiliwa, mjadala sharti uwe juu ya suala hilo lililotolewa mwisho mpaka limalizike, ndipo mjadala urudie kwenye lile suala la kwanza.

(3) Ni marufuku kwa Mbunge yeyote kuzungumzia jambo lolote ambalo langojea uamuzi wa Mahakama, au jambo lolote ambalo lilijadiliwa na Mkutano uliopo au uliotangulia na ambalo halikuletwa rasmi kwa njia ya hoja mahsusi, na vile vile ni marufuku kusema kwa lengo la kutaka kupinga uamuzi wowote uliofanywa na Bunge, isipokuwa tu kwa kutoa hoja mahsusi inayopendekeza kuwa uamuzi huo ufutiliwe mbali.

(4) Ni marufuku kwa Mbunge yeyote kuzungumzia shughuli yoyote ya Kamati ya Bunge mpaka shughuli hiyo iwe imewasilishwa Bungeni kama taarifa au ripoti ya Kamati juu ya shughuli hiyo.

(5) Ni marufuku kwa Mbunge yeyote kutumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala, au kwa madhumuni ya kutaka kushawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani.

(6) Isipokuwa tu kama kunatolewa hoja mahsusi kuhusu jambo kama hilo, itakuwa ni marufuku kwa Mbunge yeyote, katika mjadala wowote Bungeni, kuzungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Wabunge, Majaji, Mahakimu au watu wengine wanaoshughulikia na utoaji wa haki; na itakuwa ni kinyume cha utaratibu wa Bunge kugusia mienendo ya watu hao waliotajwa wakati wa hoja yoyote ya kubadilisha hoja, kuuliza swali, au wakati wa kutoa maoni juu ya hoja inayohusu jambo jingine lolote.

(7) Mtoa hoja yeyote aweza kuzungumza kwa kutaka kutilia nguvu hoja yake, lakini hakutakuwepo na mjadala wowote juu ya hoja

hiyo mpaka hoja iungwe mkono kwanza, lakini kama Bunge liko katika Kamati, hoja yaweza kutolewa na kujadiliwa bila kuungwa mkono.

(8) Ni marufuku kwa Mbunge yeyote:-

(a) kutumia lugha ya kuudhi;
(b) kutumia haki yake ya kusema kwa madhumuni ya kutaka kuchelewesha Shughuli za Bunge;
(c) kumsingizia Mbunge mwingine kuwa ana nia mbaya au kumshambulia binafsi, isipokuwa kwa kutoa hoja mahsusi inayohusu mwenendo wa Mbunge huyo;
(d) kujiingiza katika mambo ya kuwasema wenzake, au kuleta malumbano ya kisiasa ndani ya Bunge.

Marufuku kuwahisha shughuli ya baadaye

51.-(1) Itakuwa ni kinyume cha utaratibu kutoa hoja inayowahisha shughuli yoyote, ambayo taarifa yake imekwisha kutolewa, na kuwekwa katika Orodha ya Shughuli kwa siku ya baadaye.

(2) Kwa madhumuni ya kuamua kama hoja au mazungumzo yanakiuka au hayakiuki utaratibu kwa sababu ya kuwahisha shughuli za baadaye, Spika, ataangalia kama hiyo baadaye itakuwa ni ya muda mfupi au vipi kabla jambo linalohusika halijaweza kujadiliwa.

Kuzungumza zaidi ya mara moja

52.-(1) Isipokuwa tu kwa idhini ya Spika, Mbunge yeyote hataruhusiwa kusema zaidi ya mara moja juu ya hoja, ila tu:-

(a) kama wakati huo Bunge liko katika Kamati ya Bunge Zima;
(b) kama anatumia haki yake ya kujibu;
(c) kama anasema kuhusu utaratibu.

(2) Mbunge ambaye amesema juu ya hoja aweza kusema tena juu ya hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja aliyoisemea; na Mbunge ambaye amesema juu ya kutaka kufanya mabadiliko katika hoja ya awali, aweza kusema tena juu ya hoja ya awali baada ya mabadiliko kumalizika.

(3) Mbunge mtoa hoja ya msingi au mtoa hoja ya kutaka kufanya mabadiliko katika hoja iliyokwisha kutolewa, atakuwa na haki ya kujibu kabla uamuzi juu ya hoja hiyo haujatolewa. Lakini wakati huo wa kujibu, mtoa hoja atapaswa kujibu mambo yale tu yaliyozungumzwa na

Wabunge waliochangia hoja yake na hataruhusiwa kutoa maelezo yoyote mapya.

Kanuni kwa Wabunge wasio-sema

53. Mbunge aliyepo Bungeni wakati wa mjadala:-

(a) ataingia au kutoka katika Ukumbi wa Mikutano ya Bunge kwa staha na atainama kuelekea kwa Spika, au kama Mbunge mwanamke, aweza kufanya mkunjo wa magoti kwa heshima, kila mara Mbunge huyo atakapokuwa akienda au kutoka mahali pake;

(b) atatulia na kukaa kwa heshima mahali pake, na hatatangatanga katika ukumbi wa Mikutano bila sababu;

(c) hatapita katikati baina ya Kiti cha Spika na Mbunge anayesema;

(d) hatasoma kitabu chochote, gazeti au barua, ila tu kama yahusu shughuli za mjadala unaoendelea wakati huo;

(e) hataruhusiwa kutumia simu ya mkononi. Kwa ajili hiyo, atawajibika kuhakikisha kuwa simu hiyo imezimwa wakati wote.

Spika aweza kukatiza Majadiliano

54.-(1) Spika aweza kulihutubia Bunge wakati wowote, na kwa ajili hiyo aweza kumkatiza Mbunge yeyote anayezungumza. Endapo Spika atasimama wakati wa mjadala, au akianza kusema, Mbunge yeyote ambaye anasema wakati huo, au ambaye amesimama mahali pake akisubiri kuanza kusema atakaa chini; na Bunge litakuwa kimya ili Spika aweze kusikika bila matatizo.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya fasili ya (1) na ya (3), ya Kanuni hii, Mbunge anayesema hatakatizwa usemi wake na Mbunge mwingine isipokuwa kwa jambo linalohusu utaratibu. Lakini Mbunge anayesema akipenda anaweza kumruhusu Mbunge mwingine anayetaka kumkatiza kwa ajili ya kutoa taarifa ya ufahamisho juu ya jambo lililoeleweka vibaya kwa Mbunge huyo anayesema.

(3) Ni marufuku kwa Mbunge kumkatiza Mbunge anayesema isipokuwa :-

(a) kama anataka kusemea jambo linalohusu utaratibu;

(b) kama anataka kutoa hoja ya kufunga mjadala kwa mujibu wa Kanuni ya 57;

(c) kama anataka kutoa taarifa juu ya jambo lililoeleweka vibaya, na kama Mbunge anayesema atakubali na akakaa chini, na Mbunge anayependa kumkatiza akiitwa na Spika.

Taarifa kuhusu utaratibu

55.-(1) Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno "kuhusu utaratibu". Lakini Mbunge anapofanya hivyo itabidi ataje Kanuni ya Bunge iliyokiukwa. Mbunge yeyote ambaye wakati huo atakuwa anasema, papo hapo atakaa chini na vile vile Mbunge anayesimama kusemea utaratibu atakaa chini akiisha kueleza jambo hilo la utaratibu; Mbunge aliyekatizwa kusema kwa jambo la utaratibu, hatasimama kuendelea na maelezo yake mpaka Spika atakapokuwa ametoa kauli yake juu ya jambo hilo la utaratibu lililotajwa.

(2) Spika anaweza ama papo hapo kutoa uamuzi wake juu ya jambo la utaratibu lililotajwa, au kuahirisha uamuzi ili alifikirie zaidi jambo hilo na kutoa uamuzi baadaye, au kutoa uamuzi na kisha baadaye kutoa sababu za uamuzi huo, vyovyote atakavyoamua Spika. Mbunge aliyekuwa akizungumza wakati jambo la utaratibu lilipotajwa aweza kuendelea na hotuba yake baada ya Spika kutoa uamuzi juu ya jambo hilo.

Kuomba mwongozo wa Spika

(3) Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema, na kuomba "Mwongozo wa Spika" kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema katika kikao cha siku hiyo, kwa kumwomba Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge, na majibu ya Spika yatakuwa kama ilivyoelezwa katika fasili ya (2).

Kuahirisha Mjadala

56.-(1) Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye, aweza kutoa hoja "Kwamba mjadala sasa uahirishwe" na atataja anataka mjadala uahirishwe mpaka lini.

(2) Kama Spika atakuwa na maoni kwamba kuwasilishwa kwa hoja hiyo ni kinyume cha taratibu za uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge, aweza kukataa kuitoa ili iamuliwe. Vinginevyo, papo hapo atawahoji Wabunge juu ya hoja hiyo, kadri atakavyoona inafaa.

(3) Endapo hoja iliyowasilishwa itashindwa kupata kibali cha Bunge, mjadala kuhusu hoja iliyoko mbele ya Bunge utaendelea.

(4) Itakuwa ni kinyume cha utaratibu kutoa hoja ya kutaka kufanya mabadiliko katika hoja iliyotolewa kwa mujibu wa Kanuni hii.

Kufunga Mjadala

57.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni 43(6), utaratibu utakaotumika kufunga mjadala ni kutoa hoja ya kufunga mjadala, endapo bado kuna Wabunge wanaopenda kuzungumza juu ya jambo lililoko katika mjadala, au, endapo Bunge limewekewa kiwango cha juu cha muda wa kujadili hoja inayohusika, kama muda huo bado haujaisha.

(2) Hoja ya kufunga mjadala yaweza kutolewa baada ya hotuba yoyote kwisha. Hoja hiyo inaweza kuruhusiwa na Spika hata ikitolewa mara tu au muda mfupi, baada ya hoja inayohusika kutolewa kwa Wabunge ili waiamue.

(3) Mbunge anayetoa hoja ya kufunga mjadala, aweza kusimama mahali pake na kutoa hoja "Kwamba mtoa hoja sasa apewe nafasi ya kujibu". Ila kama Spika ataona kuwa hoja ya kufunga mjadala inakiuka mwenendo bora wa Shughuli za Bunge, au inavunja haki za Wabunge, Spika atawahoji Wabunge papo hapo juu ya hoja hiyo bila mabadiliko wala mjadala.

(4) Iwapo hoja "Kwamba mtoa hoja sasa apewe nafasi ya kujibu" itakubaliwa, mtoa hoja papo hapo ataanza kujibu kama akipenda, na baada ya hotuba ya kujibu kwisha, au kama mtoa hoja hapendi kujibu basi Spika papo hapo atawahoji Wabunge juu ya hoja ya awali.